

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**

Simu: +255-26-2323201-7  
Nukushi: +255-26-2323208  
Barua pepe: nje@nje.go.tz  
Tovuti: www.foreign.go.tz



Mji wa Serikali,  
Mtumba,  
S.L.P 2933  
40466 DODOMA

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**KUHUSU WATANZANIA WANAOISHI UKRAINE.**

**Dodoma, 25 Februari, 2022**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inapenda kuujulisha Umma wa Watanzania kuwa, hadi sasa hakuna Mtanzania aliyepata madhara yoyote kufuatia hali inayoendelea nchini Ukraine na kusababisha Serikali ya nchi hiyo kutangaza Hali ya Hatari (State of Emergency) tarehe 24 Februari, 2022.

Aidha, Serikali inawaomba Watanzania wote wanaoishi nchini Ukraine wakiwemo Wanafunzi, Wafanyabiashara na Wafanyakazi kuendelea kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho Serikali inaendelea kufuatilia usalama wao kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za nchini Ukraine.

Kadhalika, kufuatia kutangazwa kwa hali hiyo ya hatari, Serikali inawashauri Watanzania wanaoishi Ukraine kufanya yafuatayo:-

- i. Kufuata na kutekeleza maelekezo yote yanayotolewa na Serikali ya Ukraine kwa raia na wasiokuwa raia wa nchi hiyo;
- ii. Kuendelea kuwasiliana na Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden ambao pia unawakilisha Ukraine kwa jambo lolote la dharura kwa kufuata utaratibu wa mawasiliano uliotolewa na ubalozi; na
- iii. Wanafunzi wote waliopo Ukraine kufuata maelekezo na miongozo wanayopewa na uongozi wa vyuo vyao ikiwa ni pamoja na wazazi wa wanafunzi hao kuwasiliana na watoto wao ili kukubaliana utaratibu wa kuwarejesha pale itakapobidi kufanya hivyo.

Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu kuhusu hali za Watanzania waliopo Ukraine na inatoa rai kwa wazazi wa wanafunzi wanaosoma Ukraine kuwa watulivu sambamba na kuwataka Watanzania wote wanaoishi nchini humo kufuata maelekezo na miongozo inayotolewa na Serikali ya nchi hiyo.

Emmanuel Buohohela,  
**Mkurugenzi, Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali**